

HALMASHAURI YA WILAYA YA NACHINGWEA
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji (W))



MKOA WA LINDI:

Simu: 0732-938112

Nukushi: 0732-933112

Tovuti: www.nachingweadc.go.tz

Baruapepe: ded@nachingweadc.go.tz

S.L.P 291,
NACHINGWEA

Kumb. Na. LG.L:50/20/VOL.III/62

23/09/2019

**TANGAZO LA MAELEKEZO UCHAGUZI WA VIONGOZI NGAZI ZA
VIJJI NA VITONGOJI**

Msimamizi wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa katika Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea, anawatangazia wananchi wote wenye sifa za kugombea na kuchagua viongozi, washiriki katika chaguzi tajwa hapo juu, hii ni kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura 287 Tangazo la Serikali Na. 371 & 373 la tarehe 26/04/2019.

1. Maelekezo ya Uchaguzi

Kwa mujibu wa Kanuni za Uchaguzi huu, (Sheria ya Serikali za Mitaa) (Mamlaka za Wilaya) Sura 287 inaelekeza mambo yafuatayo:-

- (a) Tarehe ya kufanyika uchaguzi itakuwa ni tarehe 24/11/2019 siku ya Jumapili.
- (b) Muda wa uandikishaji wapiga kura; vituo vyote vitafunguliwa kuanzia saa mbili kamili asubuhi na kufungwa saa kumi na mbili jioni . Aidha kituo cha kuandikisha wapiga kura kwenye Kitongoji ndicho kitatumika kupigia kura.
- (c) Siku ya uchaguzi, kituo kitafunguliwa kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa kumi jioni.
- (d) Wakazi wote wenye sifa za kupiga kura washiriki uchaguzi .
- (e) Wakazi wenye umri wa Miaka ishirini na moja (21) au zaidi wanaotaka kugombea nafasi ya Uenyekiti wa Kijiji, Ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji, Viti Maalum Wanawake na Uenyekiti wa kitongoji wachukue fomu za kugombea zitakazopatikana kwenye ofisi ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi (Ofisi ya Mtendaji wa Kijiji).

- (f) Tarehe ya kuchukua Fomu ya Kugombea Uongozi ni siku 28 kabla ya uchaguzi ambayo ni tarehe 29/10/2019. Mwisho wa kurudisha fomu za maombi ya Kugombea Uenyekiti wa Kijiji, Ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji/Viti Maalum Wanawake na kitongoji ni tarehe 04/11/2019 saa kumi jioni ili kuanza kwa zoezi la uteuzi kufanyika baada ya hapo fomu hazitapokelewa ili kuruhusu kufanyika uteuzi wa wagombea kutokana na fomu zilizowasilishwa.
- (g) Siku ya uteuzi itakuwa ni tarehe 05/11/2019 na fomu za wagombea wenye sifa na wasio na sifa zitabandikwa mahali pa matangazo ili wapiga kura wazione.
- (h) Muda wa kutoa pingamizi dhidi ya uteuzi wa mgombea kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ni tarehe 5 - 6/11/2019.
- (i) Muda wa kushughulikia pingamizi dhidi ya uteuzi utakuwa ni tarehe 5 - 6/11/2019.
- (j) Muda wa kupeleka rufaa kwenye kamati ya rufaa wilaya dhidi ya maamuzi ya pingamizi zilizotolewa na Msimamizi Msaidizi wa uchaguzi kwa mgombea ni tarehe 5 - 8/11/2019
- (k) Tarehe ya kusikiliza rufaa dhidi ya uamuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi utakuwa ni tarehe 05 - 09/11/2019
- (l) Kampeni za uchaguzi zitafanyika kwa muda wa siku saba (7) kuanzia tarehe 17/11/2019 hadi 23/11/2019.
- (m) Siku ya kupiga kura ni tarehe 24/11/2019 siku ya Jumapili kuanzia saa mbili kamili asubuhi mpaka saa kumi jioni
- Uchaguzi utafanyika katika Vitongoji.
 - Kila mpiga kura wa Mamlaka za Wilaya atapiga kura nne kuchagua
 - (a) Mwenyekiti wa Kijiji
 - (b) Mwenyekiti wa Kitongoji
 - (c) Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na
 - (d) Wajumbe wa Viti Maalum Wanawake
 - Kwa mpiga kura wa Mamlaka ya Mji Mdogo atapiga kura moja ya kumchagua Mwenyekiti wa Kitongoji.
- (n) Kura zitahesabiwa na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi kwenye Kitongoji ambacho uchaguzi umefanyika mbele ya wagombea au wawakilishi wao, na mgombea atakayepata kura nyingi atatangazwa kuwa mwenyekiti wa kitongoji.

Matokeo kofaa nafasi za Mwenyekiti wa Kijiji au Mgombea wa Halmashauri na Viti Maalum Wanawake yatafanzwa baada ya kuunganishwa katika ngazi ya Kijiji.

2. Sifa ya Mpiga kura
 - (a) Awe Raia wa Tanzania.
 - (b) Awe na umri wa miaka kumi na nane (18) au zaidi.
 - (c) Awe ni mkazi wa kawaida wa eneo la kitongoji,
 - (d) Hana ugonjwa wa akili uliothibitishwa na daktari anayetambulika na Serikali au Bodi ya utabibu, na
 - (e) Awe amejandikisha kupiga kura katika kitongoji au kijiji husika
3. Sifa za Mgombea
 - (a) Awe Raia wa Tanzania.
 - (b) Awe na umri wa miaka ishirini na moja (21) au zaidi.
 - (c) Awe na uwezo wa kusoma na kuandika Kiswahili au Kiingereza.
 - (d) Awe na kipato halali cha kumwezesha kuishi.
 - (e) Awe ni mkazi wa kawaida wa eneo la Kitongoji / Kijiji.
 - (f) Ni mwanachama wa chama cha siasa na amedhaminiwa na chama hicho.
 - (g) Hajawahi kupatikana na hatia kwa kosa la utovu wa uaminifu katika kipindi cha miaka mitano kabla ya tarehe ya uchaguzi huu; na
 - (h) Hana ugonjwa wa akili uliothibitishwa na daktari anayetambulika na Serikali au Bodi ya utabibu.
4. Uandaaji na Uhakiki wa Orodha ya Wapiga Kura
 - Kila mwananchi mwenye sifa ya kupiga kura atajandikisha ili kuandaa orodha ya wapiga kura katika kituo kilichopo kwenye kitongoji chake.
 - Kituo cha uandikishaji kitafunguliwa kila siku saa mbili asubuhi na kufungwa saa kumi na mbili jioni.
 - Uandaaji wa orodha ya wapiga kura utafanyika kuanzia tarehe 8 - 14/10/2019
 - Orodha ya wapiga kura itabandikwa mahali pa matangazo tarehe 15/10/2019
 - Mkazi ambaye amejandikisha katika orodha ya wapiga kura atakuwa na haki ya kukagua orodha ya wapiga kura katika muda wa siku saba tangu tarehe ya orodha hiyo kubandikwa ili kutoa pingamizi au maoni ya usahihi wa orodha tarehe 15 - 21/10/2019

- Pingamizi dhidi ya mtu alieandikishwa kuwa mpiga kura itatakiwa kuwasilishwa kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi tarehe 15-21/10/2019.
- Kubandika orodha ya mwisho ya waliojiandikisha kupiga kura ni tarehe 21 - 22/10/2019.

Kifa mwananchi mwenye sifa atimize nguzo hii muhimu katika demokrasia ya kuchagua kiongozi atakae muwakilisha katika Serikali ya Kijiji. Viongozi bora wa Serikali za Mitaa ni chachu ya Maendeleo ni haki na wajibu wako kujiandikisha, kugombea na kuchagua kiongozi bora. *Shiriki uchaguzi wa serikali za mitaa 2019.*

Nnunduma, A.
MSIMAMIZI WA UCHAGUZI
JIMBO LA NACHINGWEA.

Nakala:-

- | | |
|---------------------------------------|------------------------------|
| - Mkuu wa wilaya Nachingwea | - Kwa taarifa tafadhali ✓ |
| - Mkurugenzi Mtendaji (W) Nachingwea | - Kwa taarifa tafadhali |
| - Kamanda wa TAKUKURU (W) Nachingwea | - Kwa taarifa ✓ |
| - Vyama vya Siasa Nachingwea | - Tekelezeni |
| - Mkuu wa Polisi (W) Nachingwea | - Taarifa ✓ |
| - Afisa Usalama (W) Nachingwea | - Taarifa ✓ |
| - Watendaji wa Kata wote | - Taarifa ✓ |
| - Watendaji wa Vijiji wote matangazo. | - Bandikeni kwenye mbao za ✓ |